JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA NGORONGORO
(Barua zote zitumwe kwa Mkuu wa Shule)

Tarehe 02/12/2022

MZAZI/MLEZI WA:……

SHULE YA MSINGI……..

S.L.P……

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA SHULE YA SEKONDARI MALAMBO
WILAYA YA NGORONGORO MKOA WA ARUSHA MWAKA 2022.

1.0 Utangulizi

Ninafuraha kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii mwaka 2022. Shule ya sekondari Malambo ipo umbali wa km 96 kusini mwa makao makuu ya halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro (LOLIONDO).

Usafiri wa basi kutoka mjini Loliondo unapatikana katika kituo cha mabasi cha Wasso, nauli ni Tsh. 10,000/= na kutokea karatu ni Tsh 18,000/=.

Muhula wa kuanza masomo unaanza tarehe 09/01/2023 unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe 08/01/2023 na mwisho wa kuripoti ni tarehe 22/01/2023 ndani ya siku kumi na nne.

2.0 Mambo muhimu ya kuzingatia

2.1 Sare za shule

2.1.1 Sare ya shule hii ni ya dark blue na shati nyeupe pea 2 kwa wavulana na sketi dark blue inayofika kwenye soksi yenye mshono wa malinda madogo isiyo bana na shati nyeupe kwa wasichana pea 2. NB mtindo wa mnyonyo kwa wavulana haukubaliki.

2.1.2 Rangi ya Hijab ifanane na Sare za shule

2.1.3 Nguo za shamba; sketi ya kaki inayokaribia unyayoni pia suruali ya kaki itakayovaliwa ndani ya sketi kwa wasichana na suruali za kaki zenye mshono wa kawaida kwa wavulana (pea 2)

2.1.4 T- shirt za dark blue (aina ya form six) isiyo na maandishi, yenye nembo ya shule. (zinapatikana Malambo shuleni)

2.1.5 T-shirt ya michezo ya kijani ya mgomba/yenye nembo ya shule. (zinapatikana Malambo shuleni)

2.1.6 Tai 1 ya pundamilia rangi ya dark blue yenye mistari nyeupe zinapatikana shuleni
2.1.7 Sweta jozi/pea 2 rangi ya dark blue
2.1.8 Trakisuti rangi ya Dark blue pea (blue nyeusi)
2.1.9 Chandarua 1 kwa ajili ya kujikinga na mbu
2.1.10 Soksi nyeupe pea 2 kwa wasichana na nyeusi kwa wavulana pea 2
2.1.11 Rangi ya viatu, nyeusi kisicho na kisigino kirefu vyenye kamba na vya kamba moja kwa wasichana(Juma na Rosa).
2.1.12 Nguo za ndani pea 5
2.1.13 Taulo za kike (Pedi) pea 2 kwa wasichana
2.1.14 Viatu vya michezo kwa ajili ya siku za uwanjani

2.2 Daftari 10 (Counter books quire 3 au 4), begi la kubebea daftari, file, penseli, kalamu na mkebe wa hesabu
2.3 Nauli ya wanafunzi wa bweni kwenda shuleni na kurudi nyumbani wakati wa likizo,
2.4 Godoro futi $2\,{}^{1}/_{2}$ * 6 Tanfoam
2.5 Blanketi pea moja
2.6 Matibabu ni jukumu la mzazi,
2.7 Ndoo ya plastiki lita 10 kwa matumizi binafsi
2.8 Vyombo vya chakula kama sahani, kikombe, bakuli na kijiko vyote viwe vya bati
2.9 Taulo ya kuogea
2.10 Shuka za blue bahari jozi/pea 2
2.11 Dictionary oxford **7th edition** ya kiingereza kwa kiingereza na Mathematical tables(four figure)
2.12 Kikokotozi 1 (calculator)
2.13 Vitabu vya ziada vya OXFORD au TIE vya masomo yote tisa kwa matumizi binafsi.
2.14 Saa ya mkononi kwa ajili ya kutunza muda
2.15 Ream paper 1 kwa muhula
2.16 Ufagio wa ndani (soft broom, ufagio wa nje (hard broom) na rabber squizer

3.0 Sheria na kanuni Muhimu za Shule hii.

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria namba 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu sayansi na teknolojia yenye dhamana ya elimu nchini na ofisi ya Rais–TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na Uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni:

3.1 Heshima kwa viongozi , wazazi ,wafanyakazi wote ,wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.

3.2 Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
3.3 Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (night preparation)
3.4 Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
3.5 Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
3.6 Kutunza usafi wa mwili ,mavazi na mazingira ya shule
3.7 Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa
3.8 Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote, na
3.9 Kutunza mali za umma.

4.0 Makosa Yafuatayo Yanaweza Kusababisha Kufukuzwa au Kusimamishwa shule

4.1 Wizi
4.2 Uasherati na ushoga
4.3 Ubakaji
4.4 Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine , mirungi, kubeli, sigara, ugoro na kadhalika.
4.5 Kupigana au kupiga
4.6 Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
4.7 Kudharau Bendera ya Taifa
4.8 Kuoa au kuolewa
4.9 Kugoma,kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
4.10 Kukataa adhabu kwa makusudi
4.11 Kuwa na simu ya mkononi.
4.12 Utoro wa zaidi ya siku tisini (90).

5.0 Mambo Mengine Muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shuleni na mwanafunzi.

5.1 Medical Examination Form ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni.
5.2 Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo ,fujo, na makosa ya jinai.
5.3 Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria , kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

6.0 Tafadhali soma kwa makini maelezo /maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII

……
Aziz Amran Kaduma
MKUU WA SHULE

REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

PART A

To The Medical Officer

.....

.....

.....

Mr. & Mrs./Miss.....

Please examine the above name as to his/her fitness mentally and for a full time secondary Education. The examination should include the following categories (i-iii) each category or sub-category of which will render the applicant ineligible in case of any defects.

Pregnancy (category iv) will also render a girl candidate in eligible for the secondary Education.

i. (a) Eye-sight
   (b) Hearing
   (c) Limbs
   (d) Speech
   (e) Venereal Diseases
   (f) Leprosy
   (g) Epilepsy
ii. Neuroses
iii. Other serious diseases
iv. Pregnancy

DATE.....SIGANATURE.....

PART B

I have examined the above named and consider that he/she is fit/unfit for full time Secondary Education.

i.

a) Eye-sight.....
b) Hearing.....
c) Limbs.....
d) Speech.....
e) Venereal Diseases.....
f) Leprosy.....
g) Epilepsy.....
ii. Neuroses.....
iii. Other serious diseases.....
iv. Pregnancy.....

DATE.....SIGNATURE.....DESIGNATION.......

OFISI YA RAISI-TAMISEMI
SHULE YA SEKONDARI MALAMBO S.L.P 46 LOLIONDO

TAARIFA YA MKATABA WA UTII KWA MWANAFUNZI NA MZAZI/MLEZI

1. TAARIFA (HISTORIA) YA MWANAFUNZI

1.1 Jina la mwanafunzi ……
Jinsi (me/ke)……..umri…….
Mtaa/ Kijiji anapoishi……

1.2 Jina la Mzazi/Mlezi…….
Mji/kijiji/mtaa anapoishi ……
Mawasiriano ya mzazi/mlezi. Simu ya mkononi , Baba /mama……

2. MKATABA WA KUTO SHIRIKI MIGOMO,FUJO NA MAKOSA YA JINAI SHULENI

Mimi ……..naahidi kwamba sitashiriki migomo ya aina yeyote shuleni, sitafanya fujo zozote shuleni wala kutenda kosa lolote la jinai na nakubali kutii sheria, kanuni na taratibu na maelekezo yote nitakayopewa katika muda wote nitakapo kuwa shuleni.

Jina la mwanafunzi……
Sahihi…….
Tarehe ……

3. KUKIRI KWA MZAZI KUTOA USHIRIKIANO

Mimi ……ambaye ni mzazi/mlezi wa ……nakiri kukubaliana na sheria na kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule wakati wote atakapokuwa anasoma

Jina ……
Sahihi …….
Tarehe ……..

MUHIMU; *Fomu hii ijazwe na kurudishwa shuleni*